



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Kumi – Tarehe 28 Mei, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka 2024/2025.

Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa Mwaka 2024/2025.

II. MASWALI:

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

123. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Tunampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa hatua yake ya kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa waingizaji wa sukari Zanzibar. Lengo la kuondoa VAT hiyo lilikuwa ni kupunguza bei ya sukari sokoni. Hata hivyo, licha ya nia njema ya Mhe. Rais, wananchi wengi bado wanakabiliwa na changamoto ya kumudu bei za bidhaa za vyakula, hasa mchele na unga, ambavyo ni vyakula vikuu nchini.

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta unafuu zaidi kwa kushusha VAT kwenye vyakula muhimu kama mchele na unga nchini.
- (b) Je, kwa tathmini ni kiasi gani cha vyakula hivi muhimu hutumika kila mwaka katika nchi yetu.
- (c) Je, Serikali ina mikakati ipi ya kuongeza uzalishaji wa ndani wa vyakula muhimu kama mchele, unga na sukari ili kupunguza tegemeo kubwa kwa uagizaji.

Wizara ya Afya:

142. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Hivi karibuni Serikali imejenga hospitali moja moja kwa kila Wilaya ili kuwasogezea wananchi wake huduma za afya kwa lengo la kuwapatia huduma bora zaidi ikiwa ni pamoja na kuondoa mrundikano wa wagonjwa vituoni.

- (a) Je, ni kwa kiasi gani miradi hii ya ujenzi wa hospitali hizi imekamilika.
- (b) Je, kwa kiasi gani lengo lililokusudiwa na Serikali limefikwa katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma na matibabu yaliyo bora na ya uhakika.
- (c) Je, ni ipi kauli ya Serikali kwa wananchi wake kuhusiana na kupatikana huduma hizi za afya kwa sasa.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

246. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe)
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Suala la kuongeza idadi ya misitu ya hifadhi ni moja kati ya mikakati ya kupambana na uharibifu wa ukataji wa miti na kupotea kwa misitu nchini.

Ni misitu mingapi ambayo Wizara yako ina matarajio ya kuiongeza kuwa ya uhifadhi, ili kuweza kuilinda misitu hiyo sambamba na kuvilinda vyanzo vya maji.

Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

33. MHESHIMIWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kijiji cha Nungwi ni moja kati ya vijiji ambavyo vina upungufu mkubwa wa maji safi na salama.

- (a) Je, sababu zipi zinazopelekea kukosekana kwa huduma hii kwa muda mrefu sasa.
- (b) Ni lini Serikali kupitia Wizara yako itawapelekea wananchi hawa huduma hii muhimu.

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:

224. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe)
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Je, utalii wa ndani unaleta faida gani kwa uchumi na utamaduni wetu.

III. HOJA ZA SERIKALI:


Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka 2024/2025.

Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka 2024/2025.

Zanzibar,
28 Mei, 2024.


(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA